



Swahili Version

# Mapitio ya Mpangilio wa Programme ya Réception na Placement (R&P) ya Marekani



**U**kika mwisho wa marudio yako Marekani, mwakilishi wa ofisi ya Réinstallation (au jamaa wako anayeishi Marekani, kama unaye) atakulaki katika uwanja wa ndege kukukaribisha. Utasafirishwa mpaka mahali salama na nyumba iliyotengwa kwa ajili yako na familia yako. Nyumba hio itakuwa na samani za msingi, vyombo vyya nyumba na ugavi wa awali wa chakula.

Muda mfupi baada ya kuwasili, utakutanana wafanyakazi wa Agence ya Réinstallation. Ofisi ya Agence ya Réinstallation itawapa **Programme ya Réception na Placement (R&P)** huduma na kukuunganisha na huduma zingine za kijamii wakati wa siku zako za kwanza 30 hadi 90 nchini Marekani.

Mfanyakazi wa ofisi ya Réinstallation yuko huko kukusaidia na atakuwa nguzo yako msingi ya mawasiliano. Wafanyakazi hao watashughulikia maslahi yako ya haraka.

Usijali kama huwezi kuwasiliana kwa Kiingereza kwa maana huduma zote za utafsiri zinazohitajika zitatolewa inavyohitajika.



Kila mtu mzima katika familia yako atapewa pesa kidogo kwa matumizi yake ya kibinagsi. Pia utapewa chakula au posho ya chakula kulingana na ukubwa wa family yako.



Wafanyakazi watakusaidia kuomba Kadi ya Sécurité sociale, ambayo ni muhimu kupata ajira na faida zingine nchini Marekani. Watakusaidia kujisajilisha katika huduma za ajira ambazo zitakusaidia katika shughuli zako za kutafuta kazi. Kutafuta, kupata

na kuhifadhi kazi itakuwa muhimu kwa maisha ya badaye na kujikimu kwa familia yako. Kuajiriwa ni njia ya haraka zaidi ya Auto suffisance na inayohitajika kwa mafanikio.



Mafunzo ya shule kwa watoto wote ni lazima Marekani. Utasaidiwa kusajili watoto wako katika shule ya umma, ambayo ni bure.

Huduma zote za mchakato wa uhamiaji ni bure. Kwa wakati wowote katika mchakato haistahili mtu ye yeyote kuomba malipo kutoka kwako kwa huduma yoyote. Ikiwa mtu ye yeyote atakuitisha pesa, kukulazimisha kufanya ombi, kudai kuwa anaweza kuingilia kati au kuharakisha ombi lako, au kukutishia kwa namna yoyote, tafadhalri ripoti hii kwenye Kituo chako cha Usaidizi wa uhamiaji.

Iwapo wewe na familia yako hamzungumzi Kiingereza, wafanyakazi wa ofisi ya Réinstallation watawasaidia na kuwasajilisha katika Darasa la mafunzo ya lugha ya Kiingereza.

Watakusaidia wewe na familia yako kupata hatua ya mwanzo ya Uchunguzi wa Matibabu na watakueleza kuhusu jinsi unavyoweza kupata na kulipia huduma za kiafya unapozihitaji. Watakusaidia pia kupata Assurance ya Matibabu kama iwapo muajiri wako hapeani, au bima ya kiserikali ya afya kama umehitimu.



Ofisi ya Réinstallation itatoa Orientation Culturelle ambayo itazingatia Orientation Culturelle uliohudhuria kutoka Centre de Support pour la Réinstallation. Orientation Culturelle utakusaidia kujifunza kuhusu jamii yako ngeni. Kutoka wakati unapowasili Marekani, unalindwa na sheria sawa zinazolinda wakazi wote wa Marekani. Utajifunza kuhusu haki na majukumu yako kama mkazi wa kisheria na jinsi ya kupata usaidizi unapouhitaji.

Katika siku za mwanzo 30 hadi 90 za kipindi cha Programme ya Réception na Placement (R&P) , wafanyakazi wa Réinstallation watafanya kazi pamoja na wewe ili kutengeneza na kutekeleza mpango wa kukusaidia kuwa Auto Suffisant. Ikiwa usaidizi wa ziada unahitajika zaidi ya zile siku 30 hadi 90, watakuunganisha na huduma zingine za kijamii au za kiserikali.



**Baada ya mwaka mmoja Marekani, wewe na familia yako ni lazima mjisajili kama wakazi wa kudumu wa kisheria. Miaka tano baada ya kuwasili, utaweza kujisajili ili uwe raia wa Marekani.**



The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**